## SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

# UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI YALIYOTOLEWA WAKATI WA KUWASILISHA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI JUNI 2012

## KITABU CHA TATU

## JUNI, 2013

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI YALIYOTOLEWA WAKATI WA KUWASILISHA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI JUNI 2012**

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ziara ya kutembelea Mikoa yote ya Zanzibar ili kuhakikisha vitambulisho vyote vinasambazwa kwa walengwa | Ziara ilifanyika kote Unguja na Pemba. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Waziri alifanya vikao na Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi, Masheha na Madiwani kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni kuwashajihisha wananchi kwenda kuchukua kadi zao zilizolimbikizana katika Ofisi za Usajili za Wilaya. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 2 | Mchango wa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi kwa Zanzibar sambamba na Mpango Mkakati wa kuendeleza uchumi wa Zanzibar | Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi wamesaidia ujenzi wa madarasa Skuli ya Unguja Ukuu, samani kwa Skuli za Kwale na Ziwani kisiwani Pemba na vifaa vya afya katika Hospitali ya Chake chake Pemba. Aidha, Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kushurikiana na Benki ya Elahly ya Oman imefungua "account" ambayo itarahisisha utumaji wa fedha na biashara. Sera ya Diaspora itatoa muongozo kwa upana zaidi ya kuwashirikisha Wazanzibari wanaoishi nje kuchangia maendeleo ya Zanzibar | |
| 3 | Utaratibu wa kutoa majibu kwa waajiriwa baada ya kufanyiwa upekuzi | Baada ya Kitengo cha Usalama wa Serikali (GSO) kukamilisha kazi ya kufanya upekuzi kwa wafanyakazi, mapendekezo yanayotokana na upekuzi huo huwa | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
| --- | --- | --- | --- |
| | | yanawasilishwa kwa kiongozi wa Taasisi husika | |
| 4 | Ufinyu wa bajeti za Mikoa na Wilaya | Mazungumzo yalifanyika baina ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na kwa mwaka wa Fedha 2013/2014, Mikoa imeongezewa bajeti yake kati ya TZS 83 milioni na TZS 356 milioni. | |
| 5 | Ufafanuzi kuhusu vigezo vinavyotumika kuzalisha idadi ya vitambulisho (wastani wa uzalishaji wa vitambulisho) | Vigezo vinavyotumika katika kuzalisha vitambulisho hutegemea na makisio ya takwimu kutoka kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Vigezo vyengine ni matokeo ya kinchi kwa mfano, wakati wa kujiunga na masomo ya elimu ya juu, wanafunzi huomba mikopo, wakati wa uandikishaji wapiga kura | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | na muamko baada ya kupata elimu sahihi ya Vitambulisho. | |
| 6 | Hati za majengo ya Ikulu | Gharama za upimaji wa majengo zimelipwa kwa lengo la kuyatafutia hati miliki. Jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja limeshapatiwa hati miliki na majengo yaliyobakia hati zake zimeshafanyiwa uhakiki na imebakia hatua ya kutiwa saini na kukabidhiwa. | |
| 7 | Jina sahihi la mradi wa majengo ya Ikulu, idadi ya majengo ya Ikulu na nyumba za Serikali pamoja mahitaji halisi ya fedha | Jina sahihi la mradi ni "Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali". Idadi ya Majengo ya Ikulu ni 15 ambao ulikisiwa kutumia TZS 10,000 milioni kwa kipindi cha miaka 10 | |
| 8 | Kunyimwa vitambulisho Wakaazi na kupewa Raia wa Kigeni. | Takwimu zimethibitisha kwamba Wakaazi hawanyimwi vitambulisho | Tatizo wananchi wenyewe hawaendi kuchukua vitambulisho |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
| --- | --- | --- | --- |
| 9 | Kufanya kazi kwa Taasisi ya Kiswahili ya Afrika Mashariki na eneo lililotengwa la Ofisi zake, Zanzibar. | Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kushirikiana na Wizara za SMZ zinafuatilia maamuzi ya vikao vya Jumuya hiyo kwa manufaa ya Zanzibar. | |
| 10 | Ukiukwaji wa taratibu za manunuzi Mradi wa Ujenzi wa State Lodges | Ofisi imeanzisha kitengo cha Manunuzi kwa lengo la kuhakikisha taratibu zote za ununuzi zinafuatwa | |
| 11 | Sababu zilizopelekea kusitiswa kwa ukarabati wa Ikulu ya Fumba | Uhaba wa fedha na maelekezo ya kushughulikia sehemu nyengine zilizohitaji matengenezo, mwaka wa fedha 2013/2014 ujenzi wa uzio utaanza. | Nyumba imeezekwa kama ni awamu ya mwanzo kwa dhumuni la kuinusuru isije kuathirika zaidi. |
| 12 | ufafanuzi juu ya ada ya mikataba (ZAN ID) | Ofisi Imefunga Mikataba Na Kampuni Ya *OTI* Ambayo Hujumuisha Huduma Za Kiufundi Na Malighafi Na Kampuni Ya *Securitree* Ambayo Hujumuisha Huduma Za Leseni Za Programu Zinazotumika Na Ofisi Na Ukaguzi | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | Wa ISO Shirika La Kuangalia Viwango Vya Kimataifa | |
| 13 | Ufafanuzi juu ya TZS. 80 milioni kwa matengenezo makubwa ya majengo pamoja na fedha zilizotengwa za ujenzi ujenzi mkubwa | Ikulu kubwa pekee inabidi kuwekwa rangi mara mbili kwa mwaka jumla ya TZS 60 milioni kwa mwaka | Fedha hizi zimetengwa kwenye kifungu hiki lakini hakihusiani na kazi kubwa kwa matengenezo ya majengo ambayo yamo kwenye mradi |
| 14 | Mmiliki halisi wa Ikulu ya Wete | Mmiliki halisi wa sasa wa Ikulu ya Wete ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewakabidhi rasmi kwa matumizi yao. | |
| 15 | Hatma ya kesi za wageni waliokamatwa na | Tangu mwaka 2007 Ofisi imekuwa ikipata shutuma za kuwasajili wageni, Ofisi imefanya | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi | jitihada kubwa ya kufanya uchunguzi wa awali juu ya washukiwa wageni na hatimae kuwasilisha taarifa zao katika Ofisi ya Uhamiaji, Ofisi ikipata majibu kama sio Watanzania hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yoyote yule aliejiandikisha kinyume na sheria ya usajili nambari 7 ya 2005. | |
| 16 | Ujenzi wa Ikulu ya Micheweni | Ujenzi wa Ikulu ndogo ya Micheweni utaanza mara tu baada ya kukamilika utatazi wa tatizo lililopo hivi sasa la madai ya Mrithi wa aliepewa Zabuni ya ujenzi huo. Aidha, fedha za ujenzi huo zimeanza kutengwa katika bajeti ya mwaka wa 2013/2014 | |
| 17 | Idadi ya Semina walizofanyiwa Madiwani | Jumla ya Semina tatu zilifanyika kwa viongozi wa Serikali za Mitaa.( i) Semina moja ya Kanuni za Baraza la Manispaa. (ii) | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | Semina moja kuhusu utawala bora katika kusimamia majukumu ya Serikali za Mitaa kwa Wajumbe wa Kamati za Madiwani za Fedha, Sheria na Afya. (iii) Semina ya Masheha na Madiwani Pemba ya kutathmini utendaji kazi wa Serikali. | |
| 18 | Kuondoshwa vikuta (vizuizi) katika njia ya Forodhani na badala yake kuwe na utaratibu wa kupita gari zenye uzito mdogo | Vikuta vya Forodhani vimeshaondoshwa na tayari kumeweka alama ya kuzuia kupita magari yasiozidi tani mbili eneo la Vuga na magari ya zaidi ya tani mbili yanayokamatwa yanatozwa faini ya TZS 10,000. Vilevile ruhusa maluum inatolewa na Manispaa kwa magari yenye uzito wa zaidi ya tani mbili kwa kazi maalum. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 19 | Kufungwa kwa barabara ya Malindi | Utekelezaji wake ulifanyika lakini haukudumu muda mrefu kutokana na mahitaji yaliojitokeza kwa jamii kufuatia ujenzi wa Hoteli (Grand Palace) kubwa ya kitalii eneo hilo na mahitaji ya Wafanyakazi wa Wizara ya Biashara na Viwanda. | |
| 20 | Mgawanyo wa mapato kati ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa | Baraza la Manispaa limefanya mazungumzo ya pamoja Baina ya Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya mji Mkongwe kujadili mapato ya Maegesho na kufikia makubaliano na Manispaa kuendelea na ukusanyaji wa mapato ya maeneo ya maegesho. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 21 | Usafi katika eneo la marikiti ya kuku pamoja na uchakavu wa vibaraza vya kuuzia samaki katika Soko Kuu Darajani | Serikali inaelewa hali ya soko la Darajani na mazingira ya soko la samaki. Soko hilo ni la zamani na limejengwa katika miaka ya 1904 na hivyo kutokidhi haja kwa hali ya sasa. Katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo Serikali imejipanga kulifanyia matengenezo makubwa soko la samaki katika mwaka wa fedha 2013/2014 ili liwe la kisasa na liweze kukidhi haja kwa wakati uliopo. | Utekelezaji wake pia utawashirikisha wafanyabiashara wenyewe pamoja na kuimarisha miundo mbinu ya maji safi na michirizi. |
| 22 | Kutokuwepo kwa vyoo katika kituo cha gari cha Darajani | Vyoo katika eneo Darajani tayari vipo na vinatoa huduma katika eneo hilo kwa malipo ya bei nafuu. | |
| 23 | Uchakavu wa barabara ya Mkunazini | Matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Mkunazini traffic Light yamefanyika kupitia mfuko wa Maendeleo wa Jimbo la Mji Mkongwe (CDF). | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 24 | Usumbufu unaosababishwa na Masheha katika kutoa huduma kwa jamii | Serikali imeendesha Semina elekezi kwa watendaji wa Serikali za Mitaa na Masheha juu ya uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, Kupitia vikao vya kawaida vinavyofanyika kila wiki baina ya uongozi wa Wilaya na Masheha navyo huwa vinasisitiza uwajibikaji wa Masheha kwa wananchi. | |
| 25 | Uchakavu na udogo wa Ofisi ya Baraza la Mji Wete | Hatua za ukarabati wa jengo zimefanyika. Jengo hilo pia limo katika mpango wa utengenezaji wa majengo ya Mabaraza ya Miji Pemba kupitia Mradi wa ZUSP. | |
| 26 | Kuongeza vyanzo vya mapato vya Mabaraza ya Miji pamoja na kuweka wazi mipaka yao | Sheria mpya ya Serikali za Mitaa itaainisha vyanzo vipya vya mapato kwa Serikali hizo. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
| --- | --- | --- | --- |
| 27 | Matengenezo ya barabara ya Soko la Chake Chake | Matengenezo ya barabara ya soko la Chake Chake yamefanyika katika kiwango cha lami. Aidha, sehemu iliyobakia kutoka Hospitali Chake mpaka Tibirinzi itafanyiwa kazi katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 | |
| 28 | Uzururaji wa wanyama ovyo katika Manispaa ya Zanzibar | Operesheni maalum ya kuwaondosha wanyama wanaozurura ovyo Mjini inaendelea. Jumla ya wanyama 190 wanaozurura ovyo wamekamatwa na kupelekwa katika maeneo maalum yaliyotengwa. Utaratibu maalumu umewekwa wa kuwagomboa wanyama waliokamatwa. Wanyama wote waliogombolewa huwekwa rangi maalum na pindipo akikamatwa tena hatua za kisheria huchukuliwa dhidi ya Mmiliki. | Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na “Operation Rejesha Nidhamu” inayosimamiwa na Mheshimiwa Mkuu wa mkoa Mjini Magharibi na hadi sasa operesheni wamekamata ng'ombe 68 Mbuzi 58 na Punda 7. |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 29 | Ujenzi wa choo katika eneo la Michenzani (Sunday Market) | Eneo la kujenga choo tayari limeshapatikana na Ujenzi wake unatarajiwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014 na gharama zote zitafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB). | |
| 30 | Vifaa vilivyosaidiwa katika Skuli ya Mahuduthi na Skuli ya Secondary Kengeja pamoja na shughuli za maendeleo zilizopangwa kufanywa katika Wadi ya Kisiwa Panza, Chokocho, Kangani, Mtambile, Kiwani na Mkanyageni | Vifaa mbali mbali vilitolewa kwa ajili ya kusaidia shughuli za maendeleo katika Wadi husika kama ifuatavyo:- Kisiwa Panza Bati 70, Kangani saruji pkt 70,Wadi ya Mtambile saruji pkt 70, Wadi ya Kiwani saruji pkt 30 na bati 35, Mkanyageni saruji pkt 40, bati 20 na Nondo 10. Skuli ya Sekondari Kengeja bati 30, Mahuduthi saruji pkt 20, Chokocho Saruji pkt 30 na nondo 20, Gari 2 za mawe na chokaa pkt 10. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 31 | Urasimu katika kupata leseni | Leseni hutolewa kwa mfanyabiashara ambae amejaza fomu, kukagaliwa aina ya biashara yake, kufanyiwa tathmini ya malipo na kulipa kiwango kinachohitajika kutoka na biashara hiyo | |
| 32 | Kuchelewa kwa ajira katika Halmashauri za Pemba | Tayari utaratibu wa ajira umeshakamilika. Kwa sasa Halmashauri zote zimepatiwa wanasheria, maofisa mipango na maofisa mapato | |
| 33 | Upungufu wa vifaa vya kuzolea taka Baraza la Manispaa | Tayari baadhi ya vifaa vya usafi na magari ya kuchukulia taka pamoja na maji machafu vimeshafika nchini kupitia Mradi wa ZUSP. | |
| 34 | Hatua iliofikia sera ya TAMISEMI | Sera ya Serikali za Mitaa imekamilika na imeshawasilishwa kwa wadau wakiwemo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sera hiyo kwa sasa inaendelea | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | kutekelezwa na Kamati ya Wataalamu wa kusimamia uharakishwaji wa kutekeleza sera hiyo. | |
| 35 | Sheria iliowapa Masheha mamlaka ya kukusanya mapato sambamba kifungu kinachoingia mapato hayo | Sheria Namba 1 /1998 kifungu 17 (1) (c) imempa Sheha uhalali wa kukusanya mapato ya usafirishaji wa mazao ya chakula na msitu. | |
| 36 | Kuondoshwa dampo katika eneo la Darajani, Mombasa na Mwanakwerekwe | Kutokana na mazingira ya Mji wetu na eneo la Darajani lilivyo, itakuwa vigumu jaa hilo kulihamisha kutoka sehemu hio, Taka zote kwa sasa zinakusanywa na kuwekwa moja kwa moja katika gari maalum lenye kuhifadhi taka (compactor truck), kazi hio huwa inaanza saa 1.00 kamili za asubuhi hadi saa 12.00 za jioni. Utaratibu huu umewezesha kuondosha kabisa mrundikano wa taka | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | zinazotupwa chini katika eneo hilo na harufu mbaya iliyokuwepo zamani. | |
| 37 | Uwepo wa wafanyabiashara wadogo wadogo nje ya soko la Mwanakwerekwe pamoja na kupatiwa elimu juu ya athari za barabara | Elimu ya kuelimisha wafanya biashara imetolewa na Operesheni maalum inayosimamiwa na Mkuu wa Mkoa zimefanyika kuwaondoa wafanya biashara hao na vile vile eneo limeimarishwa kwa kuekwa sawa na kushindiliwa kwa fusi kwa ajili ya matumizi ya maegesho ya gari yatakayosimamiwa na Halmashauri ya Magharibi. | Wafanyabiashara wadogo wadogo wamepatiwa nafasi katika soko la Mombasa. |
| 38 | Ongezeko la mishahara ya Baraza la Mji Wete | Suala la ongezeko la mishahara limepatiwa ufumbuzi na tayari wafanyakazi wamepatiwa tafauti zao za mishahara. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 39 | Uchafu katika misingi | Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na kikundi Maalum cha vijana kimesaidia kusafisha misingi katika maeneo ya Miembeni jitini, Kwa Chimbeni, Migombani, Jengo la Mamlaka ya Mapata (TRA) Gulioni, UUB, Jangombe Gengeni na Mwembeladu na maeneo mengine. | Misingi iliyosafishwa ni Miembeni jitini, Kwa Chimbeni, Migombani, TRA Gulioni, UUB, Jang'ombe Gengeni, Mwembeladu na maeneo mengine. |
| 40 | Soko la Micheweni kugeuzwa Ofisi pamoja na kukodishwa watu wengine | Mara baada ya jengo la soko la Micheweni kuanguka juhudi za maksudi zilichukuliwa na kuanzishwa jengo jengine kupitia ufadhil wa USAID. Jengo hilo linatumika kwa shughuli mbali mbali. | |
| 41 | Kamati ya Ulinzi ya Mkoa kuimarisha ulinzi katika eneo la Mesi ya Jeshi Dunga | Taratibu zinaendelea kwa kushirikiana na jeshi husika JWTZ kuweka usalama katika eneo hilo | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 42 | Malipo ya mara mbili (Double payment) pamoja na kutokupewa risiti za malipo kwa wafanyabiashara wa soko la Mwanakwerekwe (400,000 kwa vibaraza na 1,000 kwa risiti kila siku) | Wafanyabiashara wameelimishwa na wamefahamu kuwa malipo waliolipa ya TZS 400,000 yalikuwa ni gharama za ujenzi za vibaraza ambazo amelipwa Mkandarasi na hakuna malipo ya Double Payment. Malipo ya 1,000/- ni kwa ajili ya usafi na risiti zake huwa zinatolewa kwa kila anaelipa. | |
| 43 | Kupewa posho Madiwani | Kwa mujibu wa Sheria Namba 3/1995, Waheshimiwa Madiwani hawana mishahara. Huwa wanalipwa posho la vikao vya Kamati na wakati wa vikao vya Baraza kuu. | |
| 44 | Misingi ya maji machafu ya Mpendae | Marekebisho ya misingi ya maji ya mvua ya Mpendae ya Barabarani itakamilishwa ujenzi wake kufuatana na mpango wa matengenezo wa barabara unaosimamiwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 45 | Show rooms za Mkoa wa Mjini Magharaibi zimekodishwa au zimeuzwa na ujenzi wa Ofisi utakamilika lini | Eneo hili sio Show room na eneo hili halijauzwa wala kukodisha. Hatua inayoendelea ni kutengeneza hatimiliki ya Mkoa na andiko la Mradi ili kuanza hatua ya ujenzi | |
| 46 | Ufafanuzi kuhusu elimu iliyotolewa ya tatizo la kupasi kwa wanafunzi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na eneo lililonunuliwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A" na mmiliki wake | Mkoa umetoa elimu ya sababu za kufanya vibaya katika mitihani ya taifa na zipo changamoto zinazokabili kama vile upungufu mkubwa wa walimu wenye sifa, vifaa, maabara, maktaba, usafiri upungufu wa vyumba vya kusomea,idadi kukubwa ya wanafunzi katika madarasa, mashirikiano madogo baina ya wazazi na walimu.Aidha fidia kwa kiwanja kinachojengwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika kijiji cha Biboni Moga zimeshalipwa TZ 1500,000 | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 47 | Idadi na majina ya walioajiriwa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja katika kipindi cha miaka miwili nyuma | Jumla ya wafanyakazi wanane wameajiriwa katika kipindi cha mwaka 2011/12 | |
| 48 | Idadi ya migogoro iliyotatuliwa na iliokuwa haijatatuliwa na sababu zake | Mkoa wa Kaskazini Unguja unajumla ya migogoro 20, minane imetatuliwa, minne ipo Mahakamani na minane inafanyiwa uchunguzi | |
| 49 | Sababu ya Mabaraza ya Miji kukusanya mapato kidogo ukilinganisha na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Mabaraza ya miji yana maeneo madogo ukilinganisha na maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, hii ni kutokana na kwamba Wilaya ya Micheweni haina Baraza la Mji ambapo eneo lote la Wilaya hiyo ni Halmashauri inayo husika | |
| 50 | Kutokupewa kipaumbele kwa | Manispaa linatoa kipaumbele kwa ajira mpya | Baraza la Manispaa |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | watu waliokuwa washalitumikia Baraza la Manispaa wakati wa ajira mpya | kwa watu waliotumika Manispaa lakini suala la ajira kwa sasa limesita. | kwa sasa linaajiri watumishi wataalamu |
| 51 | Hatua iliofikia ya uwekaji wa taa za barabarani katika Manispaa ya Zanzibar | Hadi sasa, taa zinazotumia nguvu za jua zimeshawekwa katika barabara za Michenzani, Darajani, Bandari hadi Bwawani kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. | Lengo ni kukamilisha barabara zote kuu. |
| 52 | Gharama kubwa za ununuzi wa CD Mkoa wa Kusini Pemba | Fedha hizo zilikusudiwa kununuliwa Moving Camera na sio CD kama zilivyokuwa zinaonekana. | |
| 53 | Kupunguza msongamano wa watumiaji wa soko la Mwanakwerekwe | Jumla ya wafanyabiashara 310 waliokuwa wakifanya biashara zao nje ya Soko la Mwanakwerekwe wamehamishiwa Katika soko la Mombasa kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kwa lengo la kupunguza msongamano katika Soko hilo | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 54 | Hatua iliofikia ya mazungumzo baina ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Uwanja wa Amani juu ya kuwaondoa wauza magari kwenye yadi | Mkoa umo katika utaratibu wa kuwapatia eneo jengine kwa upande wa kusini wa jengo la Kampuni ya Bombay Bazaar | |
| 55 | Hatua iliyofikia ya ujenzi wa soko la Baraza la Mji Chake-Chake, Machomanne na soko la matunda. | Hatua iliyofikiwa ni kuezeka paa na milango iliyokodishwa watamalizia wafanya biashara waliokodishwa | |
| 56 | Sheria ya Serikali za Mitaa moja, mbili au tatu | Sheria za Selikali za Mtaa ni mbili nazo ni Sheria Namba 3/1995 ya Baraza la Manispaa na Sheria Namba 4/1995 ya Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji | |
| 57 | Kuhakikisha suala la upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari kwa kila raia | Jitahada zinafanyika kuhakikisha wale wote wanaostahiki na wametimiza masharti ya usajili kulingana na Sheria, wanapatiwa vitambulisho | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | wa Zanzibar ambae ana haki ya kupata kitambulisho | | |
| 58 | Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeagizwa kusimamia fedha za viburudishaji zilizopo katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji na kujiridhisha kama kweli fedha hizo zinahitajika kwa madhumuni yaliokusudiwa. | Kifungu hichi kilikuwa na jumla ya TZS 30 milioni. Kuzidi kwa kifungu hichi ulitokana na kuingizwa mshahara wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Pemba ambazo zilikuwa ni jumla ya TZS 13 milioni. Fedha hizo kwa sasa zimehaulishwa na kupelekwa katika kifungu cha mishahara katika Ofisi ya Afisa Mdhamini – Pemba. Kwa sasa kifungu hicho kina jumla ya TZS 7.5 milioni baada ya punguzo la kununua meli. | |
| 59 | Gharama zilizotumika kwa ujenzi wa Hospitali ya KMKM | Hadi hatua iliyofikiwa kwa sasa, Mradi huu umegharimu jumla ya TSZ 1,050 milioni | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 60 | Kutokutengewa fedha za michezo JKU, Zimamoto na KVZ | Idara Maalum za SMZ huwa zinatengewa fedha za michezo katika bajeti zao ambazo fedha hizo huwa hazitoshelezi mahitaji halisi | |
| 61 | Mazingira finyu ya malazi kwa Askari wa Zimamoto wa Uwanja wa Ndege Pemba | Matengenezo ya sehemu ya makaazi ya Askari wa Zimamoto katika Uwanja wa Ndege Pemba yanatarajiwa kuanza kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 baada ya kupata ridhaa ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambao ndio wamiliki wa Jengo hilo | Matengenezo madogo madogo ya Ofisi yao yamefanyika. |
| 62 | Ufinyu wa bajeti ya Chuo cha Mafunzo | Idara ilifanya mazungumzo na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na hatimae baadhi ya vifungu viliweza kuongezeka. Mfano kifungu cha chakula kutoka TZS 400 milioni kwa mwaka 2011/2012, TZS 750 milioni kwa mwaka 2012/2013 na TZS 850 milioni kwa mwaka wa fedha 2013/2014 | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 63 | Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeahidi kuchukua jitihada za kuondosha mtondoo katika Vyuo vya Mafunzo | Tayari katika Chuo cha Mafunzo cha Kangagani, Tungamaa, Hanyegwa Mchana, Ubago na Langoni wanafunzi wanatumia vyoo ambavyo vimetengwa na vyumba vya kulalia (Cells zao). | Vipo baadhi ya Vyuo kwa mfano Kiinua Miguu na Wete inakuwa vigumu kujenga vyoo kutokana na mfumo wa ujenzi uliotumika ni wa kizamani |
| 64 | Majukumu ya Vikosi vya SMZ kama ni wazalishaji, wahudumu au ni watoa huduma | Idara Maalum za SMZ zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria zilizoanzisha Taasisi hizo. Aidha, kwa mujibu wa Sheria hizo, Jukumu la Ulinzi na Usalama ni wajibu wa Idara Maalum zote za SMZ | |
| 65 | Ufafanuzi wa bajeti za ununuzi wa gari mbili za kuzimia moto | Kwa mwaka wa Fedha wa 2012/2013, jumla ya TZS 222.3 milioni zilitengwa kwa ajili ya kununulia gari nne, moja ya kubebea | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | wagonjwa na tatu ni za kuzimia moto. Gari hizo tayari zimeshanunuliwa na tayari zinafanya kazi. | |
| 66 | Kutokufatwa kwa sheria ya manunuzi katika Idara Maalum za SMZ | Kwa sasa Idara Maalum zote za SMZ zimeshaunda Bodi za Zabuni na tayari zinafanya kazi | |
| 67 | Madai ya mikato ya fedha kwa Wapiganaji | Idara Maalum za SMZ hazina utaratibu wa kuwakata Askari na wapiganaji wake. Kwa mujibu wa Sera, Wapiganaji wanachangia kiasi kidogo sana kwa ajili ya michezo wakiwa ni wanachama wa vilabu vyao | |
| 68 | Aina ya zana zilizonunuliwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 katika kikosi cha Zimamoto pamoja na sababu za kutokuwepo kwa bajeti ya | Kikosi cha Zimamoto kimenunua vipuri na vitendea kazi vikiwemo; Foam compound, Co2, Delivery Horse 35 na B.A. Pia, kimenunua jumla ya gari tatu za kuzimia moto na gari moja la kuchukulia wagonjwa. Jitihada zinaendelea | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
| --- | --- | --- | --- |
| | uokozi wa vyombo vya bahari unapotokea | kuchukuliwa kuweza kununua boti ambayo itatumika kwa kuzimia moto kwa vyombo vya baharini pindi unapotokea. | |
| 69 | Hati miliki ya Chuo kipya cha Mafunzo Hanyegwa Mchana ili kuindosha mzozo uliojitokeza baina ya Wananchi | Idara tayari imeshalipa gharama za hati miliki na sasa inasubiri tu kukabidhiwa hati hiyo. | |
| 70 | Hatua iliofikia ya ujenzi wa Chelezo cha KMKM | Kwa hatua ya awali uongozi wa KMKM umeshakaa na watendaji wakuu wa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kujadiliana namna ya kuanzisha mradi huo. Makubaliano yaliyofikiwa ni kuanza kazi ya andiko kwa ajili ya upembuzi yakinifu. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 71 | Malipo ya wanakijiji wa Hanyegwa Mchana kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo | Idara inafanya uhakiki wa kutambua gharama hali za fidia wanazodai wanakijiji wa eneo hilo. Taratibu za malipo zitaanza kufanywa baada ya uhakiki huo kukamilika | |
| 72 | Hatua iliofikia ya mazungumzo baina ya Kikosi cha Zimamoto na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege kuhusu ujenzi wa Ofisi/bweni la Kikosi cha Zimamoto katika eneo la uwanja cha ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume | Mazungumzo na Mamlaka husika yameshafanyika na michoro kwa ajili ya kituo hicho imeshawasilishwa kwa hatua za utekelezaji. | |
| 73 | Hatua iliofikia ya mazungumzo baina ya Kikosi cha Zimamoto na Kampuni | Mazungumzo yameshafanyika na Idara ya Zimamoto na Uokozi itawasilisha makisio ya gharama za utekelezaji wa ununuzi wa magari hayo. | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | ya IFECS ya Ujerumani kuhusu uwezekano wa kukipatia magari madogo land rover pamoja na vifaa vya kisasa vya DSPA vya kuzimia moto mkubwa kwa kutumia maji kidogo | | |
| 74 | Hatua iliofikia ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto Bandarini | Ujenzi wa kituo hicho utafanywa na Mamlaka ya Bandari na tayari eneo limeshapatikana | Kituo tayari kimeanza kutoa huduma |
| 75 | Hali ya kutumia faragha wakati wa upekuzi katika Chuo cha Mafunzo | Kwa sasa wanafunzi na mahabusu hawapekuliwi hadharani. Sehemu maalum (chumba) za kufanyia upekuzi kwa Vyuo vya Kiinua miguu kwa Unguja na Wete kwa Pemba zimetengwa | |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 76 | Fedha za mradi wa mboga mboga wa JKU zimeagizwa zisitumike mpaka baada ya utafiti kufanywa. | Fedha za Mradi huo hazijatumika kama ilivyoagizwa na Baraza la Wawakilishi. Aidha, Kamati ya wataalamu iliyoongozwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo iliundwa kuchunguza uendeshaji, usimamizi na faida zinazopatikana kutoka katika Mradi wa Shamba la Mfano la Pamoja linaloendeshwa kwa ubia kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Misri. Kamati hiyo tayari imeshamaliza kazi na ripoti ya uchunguzi huo imeshatolewa ambayo imetoa mapendekezo juu ya namna ya kukabiliana na changamoto zilizobainika. | |
| 77 | Askari wa Vyuo vya Mafunzo kupewa fedha za likizo kwa mpangilio maalum kwa kila | Tayari askari wanaokwenda likizo wanapatiwa fedha za likizo kufuatana na Utekelezaji wa agizo la malipo ya pesa za | Mfanyakazi atalazimika kulipwa fedha za likizo kila |

| NAMBA | HOJA | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | askari atakaekwenda likizo ukifika muda wake | likizo ambapo kwa sasa kasma ya fedha za likizo inawekwa katika bajeti | baada ya kipindi cha miaka mitatu |
| 78 | Uzimaji wa moto pindi ukitokea katika maeneo ya Mji Mkongwe | Kikosi hutumia gari ndogo zenye pump ambazo zinaweza kufika hadi kwenye sehemu ya tukio na huwa zinapatiwa maji kutoka kwenye magari yenye ujazo mkubwa (water boozer) na kufanikisha uzimaji wa moto katika maeneo hayo. | |